**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA KAMATI YA MAWASILIANO NA UJENZI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA USIMAMIZI ( UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI) WA MAFUTA NA GESI ASILIA, KUANZISHA MAMLAKA YA UDHIBITI WA SHUGHULI ZA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA, KUANZISHA KAMPUNI YA MAENDELEO YA MAFUTA NA KUHAKIKISHA UWAJIBIKAJI WA TAASISI ZA MAFUTA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NAYO

**Mheshimiwa Spika,**

Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa mzima wa afya ili kuweza kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Mswada wa Sheria ya Usimamizi (Utafutaji na Uchimbaji) wa Mafuta na Gesi Asilia, Kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Shughuli za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Kuanzisha Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Kuhakikisha Uwajibikaji wa Taasisi za Mafuta na Mambo Mengine Yanahosiana Nayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Pia, tunampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Makamo wa pili wa Rais kwa kuendelea kutuongoza kwa salama na amani na wananchi kuweza kuendelea na shughuli zao za maisha za kila siku bila ya bughudha ya aina yoyote , tunawaomba wananchi kuendelea kuilinda Amani iliyopo kwa ndio hazina pekee kwa maisha yetu na vizazi vyetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Pili, nikushukuru wewe pamoja na wasaidizi wako kwa kazi kubwa na makini mnayoifanya katika kutusimamia na kutuwezesha katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku hapa Barazani.

**Mheshimiwa Spika,**

Tatu, kwa niaba ya Kamati yangu ya Mawasiliano na Ujenzi hatuna budi kutoa shukurani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji,Nishati na Mazingira pamoja na timu yake ya wataalamu ikiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, ikisaidiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Nishati pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Usimamizi wa Mazingira, pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, pongezi maalum ziende kwa Ndugu Saleh Said Mbarak kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na Naibu Mwanasheria Mkuu, ambae alikua ndie "Dictionary" letu kwa upande wa utaalamu wa Sheria pamoja na ufundi wa sheria na miongozo yote kwenye fani ya Sheria. Kwa kweli Serikali yetu inayo hazina nzuri ya wataalamu katika fani hizi nilizozitaja hapo juu kwa hiyo ni vyema wataalamu hawa wakalindwa na kupewa fursa kubwa zaidi ili kuonyesha utaalamu wao kwa maslahi ya Taifa kwa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,**

Wataalam hawa wamefanya kazi kubwa sana katika kuandaa mswaada huu muhimu kwa Taifa letu, hadi kuweza kuufikisha kwenye Kamati yako hii na leo kwa heshima kubwa tunajivunia kuuleta hapa Barazani kwa kuuwasilisha ili tuweze kutoa maoni yetu ili baadae uwe Sheria, wataalamu wetu hawa inaonyesha waliangalia Sheria za Nchi mbali mbali na kuweza kuchukua yale mazuri na kuacha yote mabaya na ndio maana tukaweza kupata Mswaada huu ambao nnaamini wajumbe wote vwatauchangia na kutoa maoni yao ili kuuboresha na hatimae kuupitisha kwa nguvu zetu moja kwa maslahi mapana ya Nchi yetu kwa ujumla, na pia sisi ndio tutakaokua mabalozi wazuri huko Majimboni mwetu tutakaporudi ili kuweza kuwaeleimisha ,kwani hiyo ndio kazi kubwa itakayotukabili baada ya kuupitisha Mswaada huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu uliipa siku tano ili kuupitia mswaada huu zikiwemo siku mbili za wadau lakini kutokana na uzito na umuhimu wa Mswaada huu kamati yangu ilitumia siku nane kuukamilisha Mswaada huu, na kubwa ilikua ni kwa wajumbe kuweza kujua madhumuni ya Mswaada wenyewe lakini pia kujua Sheria zitakazotulinda , wanachi wetu watalindwa vipi na mali zao zitakazoathirika, lakini pia urejeshaji wa hali ya kawaida pale itakapotokea uharibifu wa mazingira, halikadhalika kujiridhisha kua hakutokua na matatizo wakati wa utekelezaji wake lakini kubwa kabisa la mwishio ilikua ni namna gani wananchi wetu hasa wa Zanzibar watafaidika vipi na rasilimali hii ya Mafuta na Gesi asilia wakati wa maandalizi hadi kuanza uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Nataka pia niwahakikishia Wajumbe wako wote kua Wananchi wetu wamewekewa maslahi makubwa sana kuanzia kwenye utoaji wa Vibali vyote, Leseni kupitia Kampuni yetu ya ndani (ZPDC) ambayo itakua ni wakala wa Serikali, Elimu, Ufundi, Ajira, Ushiriki wa moja kwa moja kwenye kutoa huduma kwa makampuni yatakayokuja na pia kulindwa kimazingira pale ambapo athari itajitokeza. kwa kweli iko haja ya sisi sote tuwapongeze kwa kazi kubwa walioifanya kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Nne, niwashukuru wajumbe wangu wote wa Kamati yangu pamoja na Makatibu wetu kwa kuweza kunipa msaada mkubwa wakati wote tulipokua tukiupitia na kuujadili mswaada huu muhimu kwa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya pongezi hizo sasa naomba niwataje Wajumbe wangu wa Kamati kama hivi ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Hamza Hassan Juma | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Suleiman Sarhan Said | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Abdalla Ali Kombo | Mjumbe |
| 4. Mhe. NassorSalim Ali | Mjumbe |
| 5. Mhe. Said Omar Said | Mjumbe |
| 6. Mhe. Mohamedraza Hassanali | Mjumbe |
| 7. Mhe. Bahati Khamis Kombo | Mjumbe |
| 8. Mhe. Kadija Omar Kibano | Mjumbe |
| 9. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Mjumbe |
| 10. Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu |
| 11. Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba sasa niungane na Mheshimiwa Waziri kuelezea kua mswaada huu ukipita na kua sheria utakua ndio ufunguo wa uchumi mkubwa kwa Nchi yetu na unaweza kuitoa Nchi yetu na wananchi wetu kutoka katika umaskini na kua Nchi yenye uchumi wa kati jambo ambalo litawafanya wananchi wetu kuishi maisha mzuri .

**Mheshimiwa Spika,**

Kwanza sote hatuna budi tumpongeze Rais mstaafu wa awamu ya NNE ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutupatia njia ya kuweza kuiwezesha Zanzibar kuwa na mamlaka yake yenyewe kushughulikia masuala yote yanayohusu rasilimali ya Mafuta na Gesi asilia pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo, kwani uamuzi wake wa kuupeleka Mswaada cwa Sheria ya OIL AND GAS REVENUE ACT YA 2015. Na kuanzisha Sheria ya No.2 ya 2015 ya Utawala ,Ukusanyaji na Usimamizi wa fedha za Mafuta na Gesi ,Sheria ambayo kif. 2 cha Sheria hiyo ndicho kilichoipa Zanzibar kuweza sasa kutunga Sheria ya masuala yake yenyewe kusimamia masuala hayo, na ndio maana hivi sasa tuko hapa kuifanya kazi hiyo. Kwa hiyo kwa niaba ya Kamati tunamuombea dua Mhe Jakaya Mrisho Kikwete apumzike kwa salama nyumbani na kulea wajukuu wake baada ya kulitumikia Taifa zaidi ya miaka 40 tunamombea Afya njema yeye na Mama Salma ingawa bado tutawahitaji kwa mawazo na mashauriano kila mara hasa katika kuweka sawa majadiliano yatakayojitokeza katika mustakbal wa suala hili hapo baadae kwani tunaamini amestaafu lakini bado uwezo wa kufanya kazi na kutoa ushauri anao tena mkubwa sana.

**Mheshimiwa Spika,**

Mswaada huu ni wa aina yake na ni mara ya kwanza kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutunga Sheria kwa jambo la Muungano na kutoa mamlaka kwa Baraza la Wawakilishi kuweza kutunga Sheria kwa jambo la Muungano ambalo limo nje ya mipaka yake yaani jambo la Muungano, kwani Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kifungu cha 64(2) ambapo kimetoa mamlaka kwa Baraza la Wawakilishi kutunga Sheria ambazo sio za Muungano ambazo zimo kwenye mamlaka ya Zanzibar, lakini Bunge la Jamhuri ya Muungano pia limepewa mamlaka kwa mujibu ya kifungu cha 64(1) na kifungu cha (4,c) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, kutunga Sheria ambazo ni za Muungano na zile za Tanzania Bara lakini kwa umuhimu wa suala hili nyeti la rasilimali ya mafuta ya Mafuta na Gesi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano kupitia Bunge imeona kwa sasa iko haja ya kutunga Sheria ili kuweza kuipa mamlaka Baraza la Wawakilishi kulipa mamalaka ya kutunga Sheria kwa jambo hili ambapo hadi sasa bado liko kwenye orodha ya (15) ya mambo ya Muungano na ndio maana leo hii tuko hapa kutunga Sheria hii ya mafuta na Gesi asilia hapa Zanzibar, suala hili limekua na mjadala mrefu kwa miaka mingi huko mitaani kuhusu Zanzibar kua na mamlaka katika jambo hili, kwa niaba ya Kamati yangu naomba kuwatoa wasiwasi wananchi wote wa Zanzibar kua rasilimali hii itakua chini ya mamlaka ya Zanzibar kwa asilimia 100% kwa mujibu wa kifungu cha (2) cha Sheria ya (REVENUE MANAGEMENT ACT ya 2015) ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyoipa mamlaka Zanzibar kuweza kutunga Sheria yake ya Mafuta na Gesi asilia, na kuipa Zanzibar

mamlaka ya kushughulikia rasilimali hii ya Mafuta na Gesi asilia pamoja na mambo mengine yote yanayohusiana na hayo, kwa hiyo sasa ni wajibu wetu kuichangamkia fursa hii ambayo tuliihitaji kwa muda mrefu, na kwa ushahidi Baraza hili la Wawakilishi kwa wakati huo lilipitisha kwa kauli moja Wawakilishi wote tuliokuwepo wa Chama Tawala na kambi ya upinzani, kuliondoa suala la Mafuta na Gesi asilia kuliondoa kwenye orodha ya mambo ya Muungano ili kuipa Zanzibar mamlaka ya kushughulikia masuala ya Uchimbaji wa mafuta na Gesi asilia yenyewe na leo ndio siku yenyewe.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na hayo niliyoyaeleza hapo juu, lakini bado ipo haja kubwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukamilisha mchakato wa Katiba iliyopendekezwa na Bunge la Katiba, ili wananchi wapate fursa ya kuipigia kura na kuipitisha ili iwe Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili suala la Mafuta na Gesi liwe sio tena jambo la Muungano, kwani suala hilo lilishazingatiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Au kama sio hivyo basi, Bunge la Jamhuri ya Muungano kufanya marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ili kuliondoa kabisa suala hili la Mafuta na Gesi asilia kwenye orodha ya Muungano kwani Katiba ndio yenye nguvu na hakuna Sheria yoyote yenye nguvu inayokiuka Katiba. Kwa maana hiyo, tunaiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kupeleka Bungeni marekebisho ya Katiba kwenye orodha ya (15) ya mambo ya Muungano ili kuipa nguvu za Kikatiba Sheria hii tunayoitunga hapa leo, na sio hili tu pia suala Bandari pia Zanzibar tumetunga Sheria ya Shirika la Bandari na hadi leo inatumika lakini bado limo kwenye orodha ya mambo ya Muungano sio hayo tu bali pia sualaa la TRA hadi leo limo kwenye orodha ya mambo ya Muungano lakini mapato yanayokusanywa Zanzibar yanaingia moja kwa moja katika mfuko mkuu wa SMZ.

**Mheshimiwa Spika,**

Haya ni baadhi tu ya mambo ya Muungano ambayo yanahitaji kushughulikiwa ili mambo yawe sawa kwa mujibu wa Katiba ya Muungano sasa mambo haya wakati wake umefika ili yafuate utaratibu wa kisheria, kwa maana hiyo tunamuomba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kuileta Katiba inayopendekezwa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili tuipigie kura ya maoni kwani haya yote niliyoyaelezea hapo juu ndio ufumbuzi wake utapatikana.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa ruhusa yako sasa naomba kuingia kwenye uchambuzi wa mswaada wenyewe. Aidha, naomba Wajumbe wote waujadili mswaada huu pamoja namarekebisho tuliyoyafanya kwenye Kamati kurekebisha speling pamoja, kuboresha lugha iliyotumika pamoja na kufuta na kuvibadilisha baadhi ya vifungu ili kuufanya uwe bora na kuleta maana iliyokusudiwa.

**SERA**

**Mheshimiwa Spika,**

Sisi Wajumbe wa Baraza hili tulipokabidhiwa miswaada hii ya Sheria hii tunaoijadili hatukuwa na marejeo **(SERA)** ya Mafuta na Gesi Asilia na ilituwia vigumu kufaham msingi na muongozo wa Sera ya Mafuta na Gesi Asilia, kwani suala hili ni kubwa tena linachangamoto nyingi sana za kiuchumi na kijamii sasa Sera ndio inayotoa msingi wa Sheria itakayotungwa na kuainisha ni namna gani wananchi watakavyolindwa na ni hatua gani zinahitaji kuangaliwa kwa karibu na pia kuangalia matokeo ya baadae na kuweka tahadhari huko mbele tunakoenda ili kusijekutokea migogoro, au mivutano ya jamii au kuumiza wananchi hapo baadae.

**Mheshimiwa Spika,**

Tunaishukuru Serikali yetu kupitia Waziri, Kamati yangu tumepata bahati ya kupatiwa Copy ya Sera hiyo hivi karibuni ingawa hadi leo hivi tunaijadili Mswaada huu Wajumbe wengi hawajaipata jambo ambalo sio zuri sana kwetu ,lakini pia hata sisi tuliopatiwa basi iko katika lugha moja tu ya Kiingereza kwa hiyo tunaiomba Serikali kuitafsiri hiyo Sera kwa lugha yetu ya Kiswahili ili Wajumbe na wananchi wengi tuweze kuielewa vizuri zaidi inatoa muongozo gani ili pale itakapotokea kukiukwa basi watu waweze kuelekeza Sera inasemaje.

**Mheshimiwa Spika,**

Sitaki nichukue muda wako mwingi kuizungumzia Sera kwani tayari baada ya kuipitia kwa kifupi yale mambo mengi ambayo yametolewa mongozo kwenye Sera basi yamewekewa misingi madhubuti kwenye Sheria au Mswaada huu. Kwa mfano, kuonyesha kua ni sababu au viashiria gani hadi kuweko Sera hiyo, kuweka tahadhari kwa wananchi kuhusu matumaini na matarajio ya wananchi, kutoa tahadhari kwa wananchi ili kutokuja kuigawa Nchi yetu kisiasa, kiuchumi, kijamii na kimajimbo na kuepuka mgawanyiko wowote wa kijamii kwa suala hili, lakini pia imejibu miongozo na ushauri wa viongozi na wanasiasa mbali mbali kwa nyakati tofauti kutamka kua Mafuta na Gesi yapo Zanzibar, na tupewe mamlaka ya kushughulika wenyewe. Vile vile Sera imeelezea

dalili zinazoonyesha kua hii rasilimali ipo kutokana na Nchi zilizotuzunguka kua karibu zote zimo katika harakati za utafiti na karibu zote tayari wameshagundua kua hii rasilimali ipo, na kwa hapa Zanzibar katika tafiti hizo ndio maana tayari vimeshakatwa Vitalu karibu vitano huko Baharini ambapo imeonakana dalili kubwa kua Mafuta au Gesi Ipo na ndio maana Vitalu hivyo tayari kuna Mkampuni ya Uchimbaji wa Mafuta tayari yalikwisha kutia saini makubaliano ya awali ili kupewa Vitalu hivyo kupitia TPDC ambapo walikua ndio waliopewa dhamana ya kushughulikia masuala haya hii ndio dalili ya mwanzo kua na hapa kwetu mali ipo. Lakini isitoshe Zanzibar katika miaka ya nyuma kuliwahi kufanyika utafiti na kugundulika ipo dalili ya kutosha kua rasilimali hii ipo na ndio maana tafiti zote hizo zinatupa matumaini kua mali ipo.

**Mheshimiwa Spika,**

Sera imetoa miongozo namna kushughulikia maeneo ambayo yako zaidi ya maili 200 ambayo yametambuliwa na Sheria ya  Kimataifa inayoshughulikia na kutawala maeneo ya mipaka ya kimataifa (United Nation Law of The Sea) (UNCLOS) ambapo tayari Jamhuri ya Muungano imeshapeleka maombi ya kuongeza maeneo yake kwa upande wa Bahari kuu ambapo ikikubaliwa tu ni dhahiri kwakua Sheria hii itakuwepo tayari ni moja kwa moja kua na maeneo ya Zanzibay ya huko maili tutakazoruhusiwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sisi itakua tayari tunayo mamlaka ya kuyashughulikia maeneo hayo.

Sera imetoa muongozo kua rasilimali hii ituwe na iwekewe mipango madhubuti kuanzia mapato , matumizi lakini pia kuboresha Sekta nyingine za kiuchumi ili iweze kuja kuwanufaisha vizazi vijavyo, lakini pia kutoa tahadhari kwa kuimarisha sekta nyingine, kuibua sekta mpya za kiuchumi za kiuchumi ili kuongeza wigo wa ajira na mapato, kuimarisha huduma za Afya ,Elimu ,miundombinu  lakini pia kujenga kizazi kilichoelimika kisayansi na Technologia ili kuondokana na utegemezi wa wataalamu huko tunakokwenda na kuhakikisha Nchi inapiga hatua kubwa katika Nyanja zote. Mheshimiwa Spika, nimeona niichambue kidogo tu miongoni mwa mambo mengi yaliyomo katika Sera hiyo kwa faida tu ya wajumbe wenzetu ambao hawakubahatika kuipata Sera hiyo lakini kama nilivyoeleza hapo mw2anzo mambo mengi yamezingatiwa kwenye Mswaada huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Naanza na kifungu cha (1) cha mswaada ambapo Sheria hii itaanza kutumika mara tu baada ya Waziri kuutangaza kwenye Gazeti RasminI la Serikali, Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inamshauri Waziri kuhakikisha kua mara tu baada ya Mheshimiwa Rais kuutia saini Mswaada huu basi asichelewe kuutangaza kwenye Gazeti Rasmini la Serikali

ili uanze kazi kwani, hivi sasa macho na masikio ya wananchi wote wa Zanzibar wanausubiri kwa hamu kubwa kwani utakua ndio nuru ya matumaini yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Sehemu ya pili ya Mswaada huu unaelezea ni namna gani rasilimali hii itakavyomilikiwa na Wananchi moja kwa moja kupitia kwa Serikali kwani vibali na leseni zote hazitotolewa moja kwa moja kwa kampuni yoyote itakayokuja isipokua ni lazima ipitie kwa Kampuni ya Taifa ambayo itakua ni wakala wa Serikali. Kwa maana hiyo, hakutokua na Kampuni yoyote ya nje itakayoweza kufanya jambo lolote bila ya uwakala wa Kampuni ya Serikali, hii inaonyesha wananchi ndio wamiliki wa moja kwa moja wa rasilimali hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu imeridhika sana kwani uchumi huu ni mkubwa sana Duniani kumuachia Mamlaka makubwa Waziri peke yake inaweza kuhamasisha rushwa kubwa hapo baadae, laikini Sheria hii ili kutekelezeka hata baada ya kuupitisha na kutiwa saini na Rais kuna kazi kubwa ili kuanza kutumika, kwani ni lazima mara tu baada ya kupita Sheria ni lazima iundwe Mamlaka, pia iundwe Kampuni ya Taifa ya Mafuta na Gesi asilia, lakini pia iundwe na Bodi hapo ndio itaweza kufanya kazi, lakini pia isitoshe mara tu baada ya kuipitisha Mswaada huu kua Sheria Waziri atunge Kanuni kwa haraka ili Sheria hii kuweza kutekelezeka. Kutokana na umuhimu huo, Kamati yangu inamuomba Waziri kutayarisha Kanuni haraka iwezenakanavyo ili Sheria hii iweze kufanya kazi kwa haraka, kwani uzoefu wetu kuna Sheria nyingi zilihitaji kutungiwa Kanuni lakini hadi leo hii baadhi ya Mawaziri wameshindwa kutunga Kanuni hizo jambo ambalo linazorotesha utendaji kwa baadhi ya maeneo. Pia, katika utekelezaji mzuri wa Sheria hii Waziri ametakiwa kuandaa Sera ya Mafuta na Gesi asilia tunashukuru Sera tayari ipo na kwa kiasi Fulani imekidhi mahitaji ya Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kifungu cha (6) cha Mswaada kimeelezea kazi na wajibu wa Waziri, Kamati yangu mwanzo ilikua na wasi wasi wa mamlaka makubwa aliyopewa Waziri kwenye Sheria hii lakini tumejiridhisha kua Waziri takriban karibu mambo yote atayafanya kupitia ushauri wa Mamlaka pamoja na Bodi itakayoundwa kupitia Sheria hii na hata baadhi ya maamuzi makubwa basi itabidi apate ridhaa ya Baraza la Mapinduzi. Kama inavoelezewa kwenye orodha ya kifungu hicho cha 6 na vifungu vengine katika Sheria hii, ingawa hapa tunatoa angalizo kwa Serikali kwa Sheria hii maamuzi makubwa tunaruhusu yafanywe na Serikali pekee isipokua tu pale Waziri alipotakiwa kutoa taafifa kwenye Baraza la Wawakilishi, lakini kwenye Sheria ijayo ambayo itazungumzia masuala

ya makubaliano ya masuala ya Gesi na Mafuta katika mambo ya miongozo ya , kodi matumizi na migao ya rasilimali kuna baadhi ya mambo hayo mengine itabidi lazima yapate ridhaa ya Baraza la Wawakilishi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kifungu cha (6) (2) cha Mswaada huu kama Sera inavyoelekeza kinampa majukumu Waziri kwa kumtaka kuongeza ushiriki wa jamii katika sekta hii, ikiwemo uwazi katika mambo mbali mbali hii ndio itawezakuwawezesha wananchi kujua taarifa nyingi na pia kuongeza wigo wa ushiriki wa wananchi katika Sekta hii, pia imeeleza kua atahakikisha mipaka sahihi ya maeneo yanayotumika masuala ya mafuta na Gesi asilia suala hili lina pande mbili kuna mipaka ya ndani baina ya watakaopewa vitalu na mipaka mingine ya vitalu ambavyo vimepakana na Nchi nyingine , kwa maana hiyo tunamshauri Waziri kua awe muangalifu sana pale atakapokuja kushauriwa na wakati wa ukataji na ugawaji wa Vitalu lakini vile vile kuanza mapema kuitambua mipaka ya eneo letu la Zanzibar na Nchi jirani ikiwemo ukanda wa Bahari kuu, kwani migogoro mingi Duniani baina ya Nchi na Nchi kwenye uchumi huu basi unatokea kwenye Vitalu vilivyoko mopakani jambo ambalo limepelekea vita katika Nchi hizo na nyengine hadi leo vita hizo zinaendelea na kuwaacha wananchi wasio na hatia hasa kinamama na Watoto wamekua ni wahanga wakubwa kutokana na maumbile yao kutokumudu vurugu na vita, leo katika Nchi hizo badala ya rasilimali hii kuwainua kiuchumi matokeo yake imekua ni balaa kubwa kwao kupelekea uharibifu wa mali zaao, kupata ulemavu wa maisha na wengine kupata vifo , kwa hiyo Mhe Waziri na Serikali kwa ujumla hapa ndipo kwenye mtihani mkubwa katika sekta hii ya Mafuta na Gesi asilia, lakini tunaamini viongozi wetu ni watu wenye busara kubwa akiwemo Waziri mwenyewe tunaamini jambo la mwanzo basi litashughulikiwa hilo kwa njia za Kidiplomasia kwa kushiurikiana na viongozi wenzao wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzani ili kuhakikisha rasilimali hii inakua ni neema kwa wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kifungu cha 6(2)(d) cha Mswaada huu kinaelezea kua Waziri atahakikisha uwajibikaji, uwazi na ufanisi katika kuendeleza mfumo wa usimamizi wa mapato na ukusanyaji wa kodi na mipango ya matumizi.

**Mheshimiwa Spika,**

kifungu hiki bado hakijatuhakikishia Wajumbe kua Waziri aliyetajwa katika Sheria hii kua ndie atakaekua ndie msimamizi unaohusu masuala ya mapato na utaratibu wa matumizi kwani hadi hivi sasa tunapitisha Sheria hii hatujatunga Sheria ya REVENUE MANAGEMENT ACT, ambayo ndiyo itakayotoa dhima na muongozo wa usimamizi wa

makusanyo na kodi na mipango ya matumizi yote ya fedha zitakazokusanywa katika Sekta hii, kwa hiyo kwa kua biashara hii mapato yake huanza kukusanywa kuanzia pale mwanzo tu Makampuni yanapokuja na kutia saini makuliano ya awali (Memorandum of Understanding) basi tayari fedha japo kiasi kidogo huanza kukusanywa kabla ya mapato mengine baadae ya kukodisha Vitalu, na kutokana na speedi kubwa ya Makampuni kuanza kupiga hodi basi tunaamini (MOU) hautomalizika mwaka mmoja tayari kuna makubaliano Serikali yetu itaanza kuingia kwani hivi sasa tayari baadhi ya Vitalu vya Zanzibar fedha za kodi zinaendelea kulipwa huko TPDC na mara tu tukishapisha Sheria hii itabidi pesa hizo tuanze kuzikusanya wenyewe, ndio maana Kamati yangu inashauri kua Sheria hiyo ije mapema ili kuanza kukusanya pesa hizo kwani kuanza kuingia katika mfuko mkuu wa Serikali moja kwa moja bila ya kuekewa masharti maalum zinaweza kuja kutumika kwa mambo mengine na kushindwa kutumika kwa misingi iliyowekwa na Sheria husika, lakini hapa kinachotakiwa zaidi ni nia njema ya udhibiti wa mapato na matumizi hayo kwani ukizingatia hata kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano kimo kifungu (133 na 134 ) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinachotaka kuwepo Account ya pamoja kwa makusanyo na mapato yake yatumike kwa shughuli za Muungano pamoja na maelekezo yake pamoja na ckuundwa Tume ya pamoja lakini hadi leo suala hili halikutekelezeka na ikawa ni moja ya kero za Muunguano, kwa hiyo hapa suala la kutunga Sheria ni moja na utekelezaji ni suala jingine.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaitaka Serikali kuhakikisha Sheria hii inaletwa haraka iwezekanavyo hapa Barazani ili tuipitishe kwani kila hatua katika biashara hii kuna mapato yatakayoanza kuingia Serikalini, mara tu Sheria hii itakapoanza kutumika kwani kama nilivoelezea hapo mwanzo tumeanza kuona watu wakipigana vikumbo kupiga hodi maofisini baada ya kusikia Baraza linapitisha Sheria hii, kwani ni moja ya ishara ya dalili njema kwa Nchi yetu kua Sheria bado haijapita lakini hodi hodi zimeanza.Kwani mapato yake yanaanzia kuanzia vibali vya awali, leseni, Bonas, Royality na mambo mengine hatua zote hizo ni mapato ya Mafuta na Gesi yanaanza kukusanywa, kwa umuhimu huo ndio maana kamati yangu inaona iko haja ya kuletwa kwa Sheria hiyo mapema.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile kama kinavyoeleza kif.6 (2)(g) kua Waziri atahakikisha kua kunakuwepo uwiano wa upatikanaji wa mahitaji ya ndani na usafirishaji mafuta Nje ili kuona kua wananchi wanafaidika na rasilimali hiyo hili ni jambo muhimu sana kwa uchumi wetu kwani ili sekta hii iweze kufanya kazi zake vizuri basi ni lazima kuwepo na miongozo maalum ya kudhibiti soko la ndani na lile la Nje kwani viko mifano hai kwa baadhi ya Nchi ambazo zinazalisha Mafuta lakini upatikanaji wa huduma hiyo ndani ya Nchi zao unakua ni

mgumu na hata bei inakua ni yajuu kwa hiyo kupelekea wananchi kukosa kuona faida ya rasilimali hiyo ndani ya Nchi zao na baadae husababisha vurugu na uasi kwa Viongozi wao.

**Mheshimiwa Spika,**

Sehemu hii ya tau ya mswaada ina vifungu 25 kuanzia Kifungu cha (7 hadi 32) ambavyo vinaelezea muundo wa vyombo mbali mbali vitakavyowajibika katika Sheria hii ikiwemo Mmalaka, Kampuni pamoja na Bodi, kama Sera ilivyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,**

Vyombo hivi vyote ni muhimu katika Sheria hii, lakini Kamati yangu imekua na uzoefu katika Mashirika mbali mbali ya Serikali kua hayana mamlaka kamili katika mipango yao ya kazi hasa katika miundo yao ya utumishi, lakini pia kwenye matumizi ya fedha ambazo wanazalisha kwani pesa zote huingia katika mfuko mkuu wa Serikali na hata inakua vigumu na kuchukua muda mrefu katika kupata marejesho yao ya pesa za kuendeshea kazi. Jambo ambalo hupelekea kuwapangulia kazi zao walizojipangia kwa kila awamu na wakati mwingine hupewa nusu ya zile walizopangiwa, sasa kwa Sekta hii ya mafuta na Gesi Asilia, Kamati yangu inatoa tahadhari mapema kwa wao wanafanya kazi na makampuni yenye pesa zao kila kitu kinatakiwa kiwe juu ya mstari. Vile vile, jambo jingine ni suala zima la kuiutambua miundo ya taasisi na kuweza kuwalipa stahiki zao watendaji na wataalamu katika Sekta hii kwa kutumia uzoefu wa taasisi zetu kutokuangaliwa stahiki zao. Hali ambayo, kupelekea wataalamu wengi ambao tutawasomesha kwa gharama kubwa lakini bila ya kuzingatia maslahi yao basi tutarajie kukimbiwa na wataalamu hao hapo baadae kwani rasilimali hii hivi sasa iko karibu nchi nyingi majirani zetu.

## MAMLAKA YA UDHIBITI NA (UTAFUTAJI NA UENDELEZAJI NA UCHIMBAJI MAFUTA NA GESI

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaiomba Serikali kuchekecha na kuteua wajumbe walio makini sana kwenye Mamlaka hii ambao watakua wataalamu, weledi, waadilifu na pia wawe wazalendo kwani hawa ndio watakaokua ni washauri wakuu wa masuala yote ya Mafuta na Gesi asilia kitaalam, kuanzia hatua za awali hadi hatua za uzalishaji na ukomo wa shughuli hizo . Pia, wao ndio watakaokua washauri wakuu kwa Waziri kwani mikataba na mambo karibu yote yatakayotoka kwenye Kampuni kwenda kwa Waziri basi wao ndio watakaokua washauri wakubwa wa kitaalamu kabla ya Waziri kuchukua hatua nyingine au kufanya maamuzi ya kiutendaji ikiwemo kutoa au kufuta Leseni , kuangalia na kudhibiti uzalishaji pamoja na mpango kazi wa makampuni ya uzalishaji na

uchimbaji Mafuta na Gesi Asilia. Lakini pia, kuhakikisha inasimamia ushindani ulio sawa kwa makampuni yatakayokuwepo katika uzalishaji na eneo hili ndio gumu sana kwani wakirubuniwa tu basi haki haitotendeka na ndio maana tukasema ni lazima na maslahi yao yalingane na majukumu yao kwani kazi zao zinaambatana na fitna kubwa ya fedha na rushwa, kutoka kwenye makampuni yatakayokuwepo hapa nchini lakini pia watakua na uwezo wa kutoa ushauri wa adhabu kwa wanaokiuka au wanaopinga au kuzuia utekelezaji wa Sheria hii, tunaamini maoni yetu Serikali itayasikiliza kwani ndio kilio chetu kwa manufaa ya wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika eneo hili Kamati yangu imegundua kua hadi hivi sasa wataalam tunao lakini bado ni wachache sana na wengi wao wanayo taaluma ya darasani zaidi lakini iko haja kwa hivi sasa aidha hawa tulionao au walioko vyuoni kuanza kuwapatia mafunzo ya vitendo kwenye maeneo ya uzalishaji ili kujua hasa mazingira mazima ya kitaalamu kwenye kazi yenyewe, na Wizara tulipowauliza wamejipanga vipi katika kuikabili hatua hii, ingawa walitiambia kua kuna vijana karibu 60 waku katika vyuo mbali mbali ndani na Nje ya Nchi wakusomea masuala ya Mafuta na Gesi lakini Kamati yangu bado haijaridhika kwani ckariby ya vijana wetu hao wote aidha wanajisomesha wenyewe kupitia Mkopo wa Elimu ya juu au wanalipiwa na wazee wao moja kwa moja ,lakini hadi hivi sasa wako huru kwani bado hawajaajiriwa, kwa hiyo Kamati yangu inaiomba Serikali kuhakikisha vijana hao wanaajiriwa mara tu baada ya kurudi nyumbani ili kuwadhibiti kwani hadi sasa tunahesabu ya wataalamu ambao bado hatuna udhibiti nao.

## BODI YA WAKURUGENZI WA MAMLAKA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu pia imeupitia muundo wa Bodi ya Wakurugenzi ukiiacha Mwenyekiti ambae atateuliwa na Rais kwa masharti ya Sheria hii, na wajumbe wengine watakaoingia kwa nafasi zao. Kamati yangu imefanya marekebisho na tunashukuru Mheshimiwa Waziri amekubaliana nayo kua kwa wale maafisa watakaoingia kwa nafasi zao kutoka katika Wizara tofauti tumependekeza kua **wasiwe maafisa tu** bali wawe **maafisa waandamizi** ambao watakua na uzito katika maamuzi ya vikao kwani majukumu ya Bodi hii yatakua ni mazito kwa hiyo lazima wawemo wajumbe wenye maamuzi makubwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika Mswaada huu kifungu cha (12)(h), Kamati yangu ilipendekeza neno **Afisa** liondoke na iwe **Muwakilishi** mmoja kutoka sekta binafsi, lakini pia neno **mmoja** liondoke iwe **zaidi ya mmoja** kwani katika Sekta hii mpya hapa kwetu tunahitaji watu wenye maarifa makubwa ambao wamebobea katika masuala ya biashara na kiuchumi

ambao wako nje ya Serikali na ambao kuwemo kwao kungeliweza kusaidia sana kutoa maarifa na ushauri wa kiuchumi kwa Bodi. Kwani Sekta Binafsi imejawa na wabunifu wengi ambao wamejiimarisha katika mabiashara na fani nyingine nyingi za kiuchumi, bila ya kusahau pia Waziri muhusika na Sheria hii ni vyema angaalia na **jinsia katika uteuzi** wake huo ,kwani katika Bodi nyingi hapa kwetu zimesheheni wajumbe wa **jinsia moja** tu na kuiacha jinsia nyingine ikikosa kutoa mchango wao kwa Taifa.

Kwa hiyo, kwa kua hivi sasa Nchi yetu imejaa wataalam wa fani mbalimbali wa jinsia zote basi Kamati yangu inamuomba Waziri aliangalie hilo hasa kwa kua Waziri wa mwanzo wa Mafuta na Gesi ni mwanamke kwa hiyo kamati yangu kwa mara ya kwanza Kamati yangu inatarajia kupata Bodi hii mpya itakayosheheni jinsia iliyoachwa nyuma kwa cmuda mrefu ikapewa nafasi kubwa na ikwezekana hamsini kwa hamsini. **Tunaamini Waziri atafanya ujasiri huo.**

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kifungu cha 16 naomba Wajumbe wasome pamoja na Jadueli la kwanza lililoko kwenye Uk 130 wa mswaada huu linalozungumzia mienendo ya vikao vya Bodi ya Wakurugenzi.

Kamati yangu imefanya marekebisho katika jadweli la kwanza liliopo ukurasa wa (130) na kukiiandikaupya kifungu cha (1) na kusomeka kama hivi ifuatavyo:-

1. **Bodi itakutana kikao cha kawaida angalau mara moja kwa kila baada ya miezi mitatu (3).**
2. **Bodi inaweza kukutana kikao cha dharura wakati wowote inapohitajika kufanya hivyo.**
3. **Vikao vya Bodi vitafanyika ndani ya Zanzibar, isipokuwa ikijitokeza haja ya kikao nje ya Zanzibar baada ya kushaurianana Waziri.**

**Mheshimiwa Spika,**

Marekebisho haya tumeyafanya ili kuzuia mianya ya kufanyika vikao vya Bodi nje ya nchi bila ya sababu ya msingi kwani uzoefu unatuambia ziko baadhi ya Bodi katika nchi jirani wamewahi kufanya vikao vya Bodi nchi za Ulaya bila ya sababu za msingi wakati ndani ya nchi zao kuna kumbi nyingi tu tena zenye viwango vya Kimataifa lakini kwa kua pesa ziko za kutosha basi waliamua kufanya vikao vyao hivyo nje ya Nchi. Kwa muhtadha huo, na kwa kua Sekta hii ya mafuta na Gesi Asilia ni Biashara ya Kimataifa basi watu wanaweza bila ya sababu za msingi wakaenda kufanya vikao nje ya nchi katika Nchi za Ulaya, lakini Kamati yangu bado katika marekebisho hayo tumetoa nafasi kama itabidi kufanya kikao au vikao nje ya nchi basi ni lazima wapate ruhusa ya Waziri baada

ya kuelezea sababu za msingi kwa maandishi ambazo Waziri ataziridhia, kama marekebisho yanavyoelezea.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, kwenye jadweli hilo hilo kifungu cha 11(1) kinachoelezea nafasi tupu ya mjumbe kuongezwa maneno kwa "**miezi kumi na mbili mfululizo** "baada neno ugonjwa, kwani kumekua na mifano hai kua ziko Bodi ambazo inatokezea mjumbe anakua mgonjwa zaidi ya mwaka mmoja anashindwa kuhudhuria vikao na hakuna mabadiliko yoyote yanayofanywa na kusababisha kukosa michango muhimu ya mawazo katika Bodi na kwa maumbile ya kazi za Bodi hii inabidi wajumbe kushiriki kikamilifu katika maamuzi yote ya Bodi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kifungu cha 19 (2) kinaelezea wakuu wa Idara na vitengo vingine kua watateuliwa na Bodi kwa mujibu wa vigezo na masharti mengine yanayohusiana na **Sheria inayohusiana na Utumishi wa Umma.** Katika eneo hili , Kamati yangu inahisi kua hapa ndipo kwenye tatizo kwani Mamlaka ya Bodi wakati mwingine yanamezwa na nguvu za Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwani mara nyingi kumekua na malalamiko mengi kwenye Mashirika, na Mamlaka na baadhi ya taasisi kua miundo yao ya Utumishi inachukua zaidi ya mwaka bila ya kutambuliwa na hatimae kukataliwa miundo hiyo jambo ambalo linawakosesha watendaji wetu ari ya kufanya kazi kwa ufanisi na wakati mwengine hata uwajibikaji kazini unakua mdogo kwani watu hufanyakazi huku wakiwa na madukuduku mengi mioyoni mwao. Na kupitia kifungu hiki hali itakua ndio hiyo hiyo, mfano hai hivi sasa kuna watu wamepandishwa vyeo na kukabidhiwa majukumu ya kuwasimamia wenzao lakini ukija kwenye maslahi wako sawa hii inasababisha ha nidhamu ya kazi kushuka kwenye maeneo yetu.

## KAMPUNI YA MAENDELEO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

**Mheshimiwa Spika,**

Kifungu cha 32 (1) kama alivyoelezea Waziri Kifungu hiki kinaanzisha Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi ya Taifa **(ZPDC)** ambayo itashiriki moja kwa moja katika biashara ya utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia kama wakala wa Serikali au kwa niaba ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**

Uanzishwaji wa Kampuni hii ndio matumaini makubwa kwa wananchi wa Zanzibar, kama ilivyoelekeza kwenye Sera ya Mafuta na Gesi kwani inatudhihirishia kua rasilimali

yetu hatopewa mgeni yeyote isipokua atapewa kupitia uwakala wa **ZPDC** hapa tunawapongeza sana wanasheria wetu pamoja na wataalamu wetu wa ndani ambao ndio waliotengeneza Sheria hii na kujali maslahi mapana ya wananchi wetu. Kwani ziko nchi nyingine hapo miaka ya nyuma na nyingine hadi leo ni watu binafsi ndio wanaomiliki visima vya Mafuta na kutengeneza utajiri mkubwa wakiwaacha wananchi wakiwa katika umaskini wa kutupwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kifungu cha 32(4), Kamati yangu inakubaliana na nia ya Serikali kwa Kampuni ya Serikali kumilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja na suala hili ni muhimu sana lisiachwe kwenye Sheria hii peke yake bali liingizwe kwenye ***Katiba ya Zanzibar*** hapo itakapokuja kufanyiwa marekebisho na kubadilishwa kwake basi iwe kwa ***kura ya maoni*** ili wananchi waamue, kwani inawezekana siku moja akatokea Rais mwenye tamaa akalishawishi Baraza lake la Mawaziri, pamoja na Bunge na wakairekebisha Sheria hii na kutoa mwanya kwao kununua hisa na kujitajirisha kupitia rasilimali ya wananchi, na jambo hili sio geni kwani hapa hapa Tanzania kuna baadhi ya watu waliitaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwailikisha Vitalu ili kutafuta waekezaji ili wawauzie hisa, kwa hiyo kwa uzito wa suala hili basi ni vyema maamuzi makubwa kama hayo ni lazima yawekewe masharti magumu kupitia kura ya ridhaa ya Wananchi wenyewe.

**Mheshimiwa Spika,**

Sehemu hii ya nne ya Mswaada huu, ina vifungu 79, kuanzia kifungu cha(33 hadi 109 ), Aidha, kifungu cha 33kinaelezea mgao wamaeneo ya Ardhi kwa ajili ya Vitalu vya Mafuta na Gesi Asilia kama ramani itakavyoelezea baada ya kuthibitishwa na Mamlaka na Waziri kupata idhini ya Baraza la Mawaziri, lakini kabla ya Waziri kufungua na kutangaza maeneo ya Vitalu ni vyema kama maelekezo ya Kifungu cha 34 (2 na 3) (a,b, I,ii,iii,iv,v,vi ) hadi (11) ni lazima kwanza ifanyike tathmini ya Mazingira ambapo Waziri atazingatia athari kwa jamii ikiwemo wamiliki wa maeneo yaliyokatwa Vitalu, na kuangalia fidia yao kutokana na maeneo yao kuchukuliwa na kuweza kufidiwa HAPA Kamati yangu inaomba hii fidia watakaolipwa wananchi iendane **na bei ya bei ya soko** na sio kuangalia Sheria ya Ardhi ambayo wananchi wengi wamekua wakiilalamikia sana kua haiendani na wakati kwani fidia wanayoipata wengi inawaingiza kwenye umaskini wa kudumu badala ya kuwasaidia kuendeleza maisha yao, na hili tumeliona kwenye maeneo ya uwekezaji hasa Mahoteli wananchi wengi wamebaki kua maskini kwa kulipwa fidia ndogo wakati uekezaji unaendelea kuzalisha mamilioni ya shilingi.

Kwa hiyo, ni vyema katika sheria hii ni vyema fidia kwa wananchi iwekwe kwa mujibu wa soko na sio kama ilivyo sasa, na ni vyema fidia hiyo iwe endelevu ili na wananchi

kufaidika na matunda ya uekezaji huo na ndio ushiriki bora zaidi kwa wananchi katika biashara hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kama Sera ilivyoelezea taatifa ya tathmini ya mazingira ndio itakayotoa muelekeo mzima wa hatma ya uwekezaji pia tathmini hii itatoa, mwanga kwa Maendeleo ya Taifa, Kilimo na Uvuvi utaathirika vipi na namna ya kujiandaa na changamoto zake. Vile vile, kwenye Sekta na biashara ya utalii ambayo ndio uti wa mgongo wa Taifa letu, lakini pia athari nyingine za kijamii ikiwemo uingiaji wa watu kiholela hasa watakaoingia nchini kuja kutafuta kazi, lakini pia kuthibiti mfumko wa bei wa bidhaa na maingiliano ya jamii tofauti na kulinda utamaduni wa nchi.

Pia, tathmini iangalie sana athari kubwa inayowapata hasa kinamama na Watoto hasa kwa udhalilishaji, ni vyema tathmini iangalie zaidi ni vipi kinamama wataezeshwa kujiajiri au kuajiriwa kwani bila ya kuwawekea mipango madhubuti basi watakuja kubakia masikini na kua watazamaji tu na kujikuta baadhi yao kujiingiza kwenye ukahaba kama zilivyo baadhi ya nchi ambazo zenye uchumi huu wa mafuta na Gesi Asilia, pia ni vyema kuimarishwa Shule za amali ili kuwawezesha vijana wengi kupata taaluma kuweza kuajiriwa kwenye sekta hii au kujiajiri wenyewe, ni lazima kuwekwe mafungu maalum kwa ajili ya kutoa taaluma kwa jamii kwenye uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**,

Tathmini ya Mazingira pia iangalie sana zile shughuli za kiuchumi zitakazoathirika moja kwa moja kwa wananchi wa kawaida pia na kuwaandalia shughuli mbadala za kuendeshea maisha yao pale zitakapokuja kukatishwa kutokana na uekezaji huu mkubwa katika nchi yetu, kwa mfano wenzetu Nigeria kwenye bonde la Niger Delta , bomba la mafuta lilipopasuka basi na kupelekea mto ambao wananchi wakiutumia kwa shughuli za kilimo, pamoja uvuvi hata ndege walikua wakitumia mto ule tumeshuhudia wakiuathirika na wengine kufa kutokana na kuvuja kwa bomba hilo, kwa hiyo biashara hii ni nzuri lakini pia kujiandaa na changamoto zinazokuja na haya yote yatakua mepesi ikiwa jamii itashirikishwa mapema na kupewa taaluma ya kutosha ili na wao kujiandaa na hayo mabadiliko yatakayotokezea.

## KIBALI CHA UTAFITI WA AWALI

**Mheshimiwa Spika**,

Sehemu hii imeanzia kifungu cha 33 hadi 109. Kwa kuzingatia kifungu cha 35(1) Sehemu hii inaelezea hatua mbali mbali za kuanza utafutaji wa Vibali na Leseni za vibali vya ruhusa ya uzalishashaji. Sehemu hii ndio hatua muhimu unapotakiwa usimamizi mzuri wa

Sheria kama Sera inavyoeleza kwani katika hatua hii Makampuni tayari yanakua yameshajifunga kuingia mikataba na Serikali kwa ajili ya utafiti, uchimbaji, uzalishaji na uendelezaji wa rasilimali hii na hapo na sisi wajibu wetu mkubwa ni kuangalia maslahi ya wananchi wetu kama Sera ilivyoeleza kua matumaini ya wananchi ni kua shughulu hizo wananchi wetu waanze kunufaika moja kwa moja kupitia taaluma, ushirikishwaji katika uhaulishwaji wa maeneo yao na pia kuandaliwa na fursa zitakazokuwepo kupitia uekezaji huu mkubwa hapa Zanzibar.

Katika eneo hili, Kamati yangu inaiomba tu Serikali kuangalia zaidi kwa yale maeneo ambayo yamehifadhiwa kwa ajili maalum ya hifadhi ya viumbe hai ikiwemo wanyama, misitu , na shughuli nyingine za kijamii ikiwemo maeneo ya kuzikana na mengine ya kijamii, lakini hapa hapa muhimu kuangalia ni kipi kitakacholeta tija zaidi ,tusije tukazuia kutoa Kitalu eti kwa sababu kuna vyura ambao ni adimu Duniani ,hapo kikubwa ni kuangalia tija, vile vile kama Sheria inavyoeleza kua kabla ya Waziri kutoa kibali basi ahakikishe matakwa yote ya Sheria pamoja na masharti ya Mazingira yamefuatwa ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Ni muhimu kuanzia hivi sasa kuandaa wataalamuwa kutosha katika Sekta hii kwani mara tu baada ya Sheria hii kupita basi kuna harakati kuanza kwani pia kwenye huo utafiti wa awali basi ni lazima wataalamu wetu wa ndani wathibitishe na kujiridhisha kwa kila hatua ya utafiti. Vile vile, na kuhakikisha taarifa hizo zinakabidhiwa Serikalini na kusiwe na mwanya wa kuziachia Kampuni kuziuza taarifa hizo na kujipatia mapato ambapo yalitakiwa yaingie Serikalini, na mapato hayo kama tulivyoshauri mwanzo ni vyema yakaanza kuekewa utaratibu wa kisheria ili kuhakikisha zinatumika zaidi kusomesha wataalamu pamoja na kuimarisha miundombinu ya ofisi pamoja na vitendea kazi, hasa tukizingatia shughuli hizi ni za kisayansi zaidi kwa hiyo tunatakiwa tuwe na vifaa vya kisasa ili kuweza kupata Data sahihi muda wote, pamoja kua kwa hivi sasa hatuna vifaa vya kisasa vya kuweza kukusanya taarifa za utafiti ni vyema basi tukaandaa mazingira ya kua na kituo hapa nchini ili tafiti zote zitafsiriwe hapahapa nchini na hilo tukilivalia njuga linawezekana.

**Mheshimiwa Spika,**

Pia, Sheria hii imempa mamlaka Waziri kabla ya kutoa kibali cha awali kwa Kampuni kuhakikisha yale masharti yote yaliyowekwa na Sheria hii kuangalia tathmini ya Mazingira na kupeleka mpango kazi wa Kampuni kwa hiyo kama ikiwa haya yote yatazingatiwa basi wananchi wetu watanufaika sana na uekezaji huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kama kifungu cha 49 (1) kinavyoeleza kua ni lazima Kampuni itakayopewa leseni iwe na uwezo na uzoefu katika shughuli za uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia na kusiwepo mwanya wa kuja kuipa leseni Kampuni ambayo haijawahi kufanya kazi yoyote hapa Duniani kwani hayo tumeshayashuhudia kwa baadhi ya kazi hapa kwetu kuachwa watu wenye uwezo na uzoefu na kupewa Kampuni za mikobani na matokeo yake kuitia hasara Serikali na pia kupunguza kasi ya maendeleo hapa Zanzibar. Kwa hiyo, hili ni lazima tutoe tahadhari mapema kwani Serikali ndio hapa tunaipa meno kupitia kwa Waziri, na pia tukumbuke leo tuko sisi na hatujui huko mbele wajao watakua na hisia gani kwa nchi yao bila kuzingatia matumbo yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kifungu cha 50 (1) kinaelezea hifadhi ya Vitalu katika eneo hili Kamati yangu inaishauri Serikali kuhifadhi baadhi ya Vitalu kwa matumizi ya baadae,lakini pia kufanya tathmini kubwa ya kutosha kabla ya kuvitoa ili kujiridhisha rasilimali iliyoko kiasi gani kwani kuna baadhi ya nchi walikata Vitalu vikubwa na kuwapa Makampuni na baadae waligundua kua wamewapa vitalu vikubwa kimoja kwa vitatu na kuikosesha mapato makubwa Serikali na hivi sasa wameanza kupunguza ukubwa wa Vitalu kwa kuzingatia Rasiimali iliyopo. Kwa hiyo hapa kunachangamoto kubwa hasa katika maeneo ambayo tumepakana na wenzetu Jamhuri ya Muungano a,mavyo tayari vimeshatolewa kupitia mikataba ya huko nyuma sasa tujakugundua kua vimetolewa na imeonekanwa kua ni vikubwa sana sasa hapo ndipo busara zije vkutumika ili kuhakikisha kua maslahi ya Taifa yanazingatiwa, pia Kamati yangu inashauri wakati wa ugawaji wa Vitalu hivi basi kuwapatia makampuni makubwa tofauti yenye uzoefu mbali mbali ili kuweka ushindani ulio bora na pia wataalamu wetu watapata uzoefu tofauti kutoka katika makampuni tofauti.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kua Waziri yeyote atakaekaa katika Wizara hii atakua na mtihani mkubwa wa kimaslahi hasa katika eneo la kutoa, na kuongeza muda wa Leseni hapa ni vyema Mawaziri wakawa waadilifu kwa kusikiliza na kufuata ushauri wa wataalamu kwani eneo hili ndilo linaloweza kuwafanya Makampuni yatakayokuwepo kupata usawa miongoni mwao vinginevyo wengine wanaweza kupewa upendeleo .

## LESENI

**Mheshimiwa Spika,**

Ukizingatia masharti ya Kifungu cha 51 (1)(e) moja ya masharti ya Kampuni kupata Leseni ya kuchimba Mafuta na Gesi Asilia nikuwasilisha mpango kazi wake ukionyesha ni mipango gani aliyonayo katika kutoa elimu na mafunzo kwa wazawa ili kuweza kuziba pengo la wataalamu wa kigeni kuwapisha wazalendo kushika nafasi muhimu za kitaalamu na kiufundi ambapo mpango huo utawahakikishia wazawa kuweza kuajiriwa na kushika hatamu kubwa za kiutawala, kwani tumeshuhudia nchi mbali mbali zinazochimba Mafuta na Gesi wananchi wao wamekua ni wataalamu na viongozi katika Makampuni makubwa ya Mafuta Duniani, lakini ukiacha utaalamu mkubwa pia Kampuni ionyeshe pia mpango kazi wa kutoa mafunzo ya ajira kwa wananchi wa kawaida hasa ambao wanaishi maeneo ambayo miradi hiyo inafanyika, kwa kuzingatia hayo pia Waziri amepewa nguvu kwenye kifungu cha 52(1) ili kuhakikisha wananchi wazalendo wanafaidika na kila hatua ya uekezaji huu hapa nchini.

## LESENI YA UENDELEZAJI

**Mheshimiwa Spika,**

Kifungu cha 63(1)(a – f), kimeelezea masharti ya kupata Leseni kwa Kampuni ya Serikali na Kampuni za nje katika eneo hili kumekua na hofu kubwa kwa watu mbali mbali waliosoma mswaada huu kuhusu utoaji wa Vibali vya Utafiti wa Awali, Leseni na Leseni ya uendelezaji labda kwa kuhisi kua kuna uwezekano mkubwa wa baadhi ya Makampuni kupewa Vibali vya Utafiti wa Awali na baadae kuja kuwanyima Leseni ya uendelezaji hapo baadae nadhani eneo hili tuwatie moyo wananchi kua masharti haya kamati yangu imeyakubali ili kuhakikisha kua tunapata Makampuni yenye uwezo na sio wababaishaji kwani biashara hii ni kubwa na Kampuni yoyote ikija kukata Leseni basi wataweza kufuata masharti yote ya Sheria na kuweza kuzalisha mali ya kutosha kwani hatutegemei kua zitakuja Kampuni kuomba Leseni na kutumia mapesa mengi bila ya kua na uhakika na wanachokifanya kwani kwa mujibu wa Sheria hii ukishindwa katikati ya kazi basi Serikali haitolipa chochote na chochote kilichoekezwa kitakua mikononi mwa Serikali kupitia Kampuni ya Serikali kwa hiyo wajumbe na wananchi tuone ni jinsi gani Sheria hii ilivyowajali na kuwalinda wananchi wake. Lakini pamoja na kua Kamati yangu imeridhia hatua hizo lakini pia iko haja Waziri utakapokuja kutoa ufafanuzi na kuwatoa hofu waekezaji kua hakuna matarajio ya kuipa Kmpuni kibali na baadae kuwakosesha Leseni na kibali cha uzalishaji, hili litazidi kuwatia moyo Makampuni ili kuja kuekeza Zanzibar.

Mheshimiwa Spika,

Pia, Kampuni itakayopata Leseni ya Uchimbaji na Uzalishaji itatakiwa kuonesha kujenga uwezo wazalendo kitaaluma na pia kutoa ajira kwa wananchi, kama Sera inavyotoa muongozo wa kuwawezesha wazalendo, pia ataonyesha njia za kiusalama kwa wafanyakazi na jamii zitakazotumika wakati wa dharura na hii itawaondolea hofu wananchi kwani tumeshashuhudia ajali za kuripuka visima au kupasuka kwa mabomba ya kusafirishia mafuta jinsi watu wanavyoathirika, kwa hiyo ni vyema mipango yao ikaonyesha mapema ni jinsi gani wataweza kukabiliana na majanga wakati wa dharura, kama Sera inavyoeleza.

## KIBALI CHA UZALISHAJI

Mheshimiwa Spika,

Kifungu cha 71 (1) kinaelezea namna ya Waziri atakavyoweza kutoa kibali cha uzalishaji baada ya Mamlaka kujiridhisha na hatua zote tangu Kibali cha Awali, Leseni, Leseni ya Uendelezaji na hatimae kumshauri Waziri kutoa Kibali cha uzalishaji baada ya kujiridhisha na hatua zote hizo, pamoja na kua ni mdorongo mrefu lakini Sheria hii inaonyesha ni jinsi gani Serikali kupitia Mamlaka itakavyokua makini kufuatilia kila hatua hadi uzalishaji ndio maana tukasema ni lazima Serikali kuangalia sana maslahi ya Mamlaka ili wasijekupata vishawishi kutoka kwenye Makampuni.

Mheshimiwa Spika,

Kifungu cha 72(5) kinaelezea iwapo mkusanyiko wa Mafuta unaendelea hadi nje ya mipaka ya Mamlaka ya Zanzibar Serikali itafikia makubaliano na nchi nyingine ili kuona mgawanyo wa mapato unaenda vizuri na hapa ndio pale Kamati yangu ilipoishauri Serikali mara tu baada ya Sheria hii kutiwa saini basi suala la mwanzo ni kuangalia mipaka yetu ili kuweka utaratibu mzuri wa uvunaji rasilimali hii kubwa hapa Duniani, lakini pia itazitoa hofu Kampuni mbali mbali za nje zitakazokuja kuingia mikataba na Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika,

kamati yangu imeridhika na mfumo mzima wa uwazi kwa kila hatua tangu Kampuni kualikwa na kupewa Vibali vya awali,lakini pia katika kuwajulisha wananchi kupitia tamko la Serikali kwenye Gazeti la Serikali  kama Kifungu cha 84(1 na 3) kinavyelezea hii inaonyesha ni jinsi gani walioandaa Mswaada huu walivyokua makini katika kulinda maslahi ya Umma pamoja na mpango mzima wa kazi ambapo wananchi wataweza kuitumia fursa hiyo kujipanga kutumia fursa hiyo.

## MASHARTI YA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,**

Kifungu cha 77 (1) kinaelezea masharti ya jumla ikwemo kuweka kumbu kumbu za rajisi za mikataba ya Makampuni ya Mafuta na Gesi Asili na kweka kumbukumbu za makubaliano ya mabadiliko mengine ya Mikataba, pia kifungu kidogo cha (2) kimeelezea kua Rajisi zitakua wazi kwa umma isipokua kama kuna maelekezo mengine ya kisheria pia vifungu vinavyofuata vinaelezea masharti ya haki za Mikataba mingine ya Mkampuni. Vile vile Kifungu cha 79(2)(a - j) kinaelezea kuhusu maombi ya kuhaulisha hati baina ya Makampuni ambapo Waziri anahitajika Waziri kuridhia hili ni suala jema kwani tumekua na uzoefu huko nyuma kwa wamiliki wa Mahoteli ya kitalii kuhaulishana mikataba ya hisa bila ya Serikali kujua na hatimae kuikosesha mapato Serikali.

Jingine ni kwenye kifungu cha 82 ambacho kinazitaka Kampuni kuwasilisha kumbu kumbu za ugunduzi na taarifa nyingine kwa Mamlaka ili kujua ni ugunduzi gani umeonekana na kuifanya Serikali kutoa miongozo ya nini cha kufanyika hapo baadae kutokana na taarifa mbali mbali. Pia kifungu cha 89 kinawabana Makampuni kuhakikisha uzalishaji unatosheleza soko la ndani. Aidha, kifungu kidogo cha (2) pia kinadhibiti kutokupindukia hisa ya faida kati ya Kampuni na Mkandarasi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kifungu cha 94 (1 - 3) kinatoa miongozo ya Makampuni yatakayopewa Leseni kutokuchimba chini ya masafa maalum yaliyowekwa kwenye Mikataba ili kuepusha kuja kuingiliana kusababisha uvunaji wa mafuta kutoka kwenye Vitalu vilivyokaribiana na hapo ndio mara nyingi hutoke ugomvi baina ya Nchi kwa madai ya kuibiana rasilimali hiyo, kwa hiyo hapa ni vyema Serikali ikawa makini katika ukataji na ugawaji wa Vitalu ili kuepusha ugomvi au mvutano katika jambo hili.

**Mheshimiwa Spika,**

Kifungu cha 98(1) kinaelezea kuhusu haki ya matumizi ya Ardhi kwa mkaazi halali katika eneo la uchimbaji wa Mafuta na gesi kwa shughuli za ufugaji ,kilimo au ufugaji ambao hautaathiri shughuli za Uchimbaji wa mafuta na Gesi asilia, ambapo (2) hatoruhusiwa kujenga jingo la lolote bila ya ridhaa ya ridhaa ya maandishi ya Kampuni au kama akikataa bila sababu Waziri anaweza kutoa kibali bila kuathiri maslahi ya mkaazi suala hili ni vyema wakati wa utekelezaji wake basi wahusika wawe makini katika kufikia makubaliano kwani jirani zetu wa Nchi za Afrika ya mashariki kuliwahi kutokea mgogoro mkubwa baina ya wananchi wa kijiji Fulani na Serikali kwani Serikali ilikusudia kufanya shughuli za maendeleo lakini wanakijiji walikuja juu na maisha ya watu yakapotea, kwa hiyo hiyo iwe ni kama tahadhari kwetu., (4) inaelezea Kampuni kuonyesha shughuli

zitakazoathirika ikiwemo ,uvuvi ,usafiri wa majini, nk isipokua ataijulisha Mamlaka ili kuzingatia maslahi ya wananchi, eneo hili pia ni la kuzingatia.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu haikukubaliana na Mswaada kif 99.(1) cha Mswaada wa Sheria hii kwani kwani kinaelezea kua mkaazi au mwananchi atakaeathirika au kupata hasara kwa eneo lake au mazao yake kua atalipwa fidia kwa kutumia Sheria ya usimamizi wa Ardhi iliyopo hii haitokua haki kwani Sheria yetu ya usimamizi ya Ardhi imeshapitwa na wakati kwani inaelezea kua kweli Ardhi ni mali ya Serikali na Serikali itakapoitaka kuitumia kwa shughuli za maendeleo basi mtu huyo atalipwa fidia kwa vipando au kwa kile alichokiendeleza hapo juu, ( kwa hiyo Kamati yangu inapendekeza kua mtu alipwe kwa mujibu ya thamani ya Soko kwa wakati vhusika) kwani uzoefu unatuambia hivi sasa katika ukanda wa maeneo ya utalii watu hulipwa kwa mujibu wa Soko na waekezaji wanakubali hivyo na wananchi wanafaidika, lakini kwa wale ambao walilipwa kwa mujibu wa Sheria hiyo wamerudi sana nyuma kimaenedeleo kwani Ardhi hizo walikua wakizitumia kwa kilimo kuendseshea maisha yao na familia zao.

## MRAHABA

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kifungu cha 101 kinaelezea namna ya mgawanyo wa Mapato ya Mafuta na Gesi Asilia kama inavoonekana katika Uk. 133. Mhe Spika, hapa ndipo wajumbe wako hawa pamoja na wananchi wote pamoja na wadau wengine ndipo wanapoasubiria ufafanuzi wake wa kina ili waweze kuridhika na kuona faida watakayoipata wananchi yaani **(PRODUCTION SHAREING AGREMENT)** kwa ufupi wake ni PSA.

Kwa maoni ya kamati baada ya kupata seminar kutoka taasisi tofauti na pia wataalam wa Wizara basi tumeridhia na tumeona kua Serikali itafaidika sana kupitia mgao huo na hakutokua hasara kwa Serikali kwani ktakua na mgao wa Mwanzo wa 15.5% kwa Nchi kavu na 7% kwa baharini kwa kuzingatia ugumu na uzito wa kazi hiyo ya utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi asilia ambapo huu utakua ndio mrahaba **(ROYALITY)** huu ndio utakao kua mapato ya mwanzo kwa Serikali na pili itakua ni mgao atakaojilipa Mkandarasi ili kurejesha gharama zake ( COST OIL) na Tatu wakati wa uzalishaji faida itakayopatikana katika mauzo ya mafuta au Gesi kwa kuanzia Serikali itapata asilimia hamsini kwa hamsini kuanzia mapipa 0 hadi 12,499 kwa eneo la NCHI KAVU na asilimia ya Serikali itakua inapanda kwa 5% kwa kila wingi wa uzalishaji utakavbyokua na

Mkandarasi atashuka asilimia zake 5% kwa kila zinapoongezeka za Serikali ambapo pia atalazimika kulipa kodi ya Serikali kama jadueli la pili linavyojielezea na kwa upande wa BAHARINI kuanzia mapipa 0 mapipa 49,000 Serikali itagawana faida ya 50% kwa 50% NA KILA UZALISHAJI UKIWA MKUBWA BASI ASILIMIA YA Serikali itaongezeka kwa ASILIMIA 5% na Mkandarasi asilimia zake zitapungua 5% kila zinapopanda za Serikali na mwisho Mkandarasi akishajilipa gharama zake Kitalu kitakua mali ya Serikali 100% na ikiwa Serikali itahisi kuendelea na Mkandarasi huyo kwa uzalishaji basi kutakua na masharti mengine ambayo SERIKALI itayaweka na Mkandarasi kama atayakubali kwa maana hiyo SERIKALI ITAFAIDIKA NA KUPATA Mrahaba, faida kubwa kwenye mgao wa faida na pia kodi kutola kwa MkNDARASI.

**Mheshimiwa Spika,**

Sio hivyo tu bali katika Kifungu cha 102 kinachozungumzia Kampuni na Mkandarasi watalipa ada ya leseni kwa kila mwaka na hayo pia yatakua ni mapato ya Serikalii, ambapo pia itajumuisha kodi ya eneo na ada za mafunzo na utafiti na pamoja na malipo hayo kuna malipo ya ziada ambayo Kampuni na Mkandarasi watailipa Serikalini kutokana na maelekezo ambayo Waziri ataitunga hapo baadae na kuidhinishwa na Baraza la Mapinduzi., kutokana na hayo yote ambayo nimeyaelezea ndio maana Kamati yangu imeridhika na mapato hayo ambayo yamewekwa kwenye Jadueli na miongozo mingine iliyotajwa na Sheria na Kanuni itakayotungwa hapo baadae, Mhe Spika, pamoja na Kamati kuridhika na mapato hayo yote lakini bado tunahitaji Sheria ya udhibiti na matumizi ya Fedha za Maendeleo vya Petroli ili kuhakikisha kua zinatumika kwa masalahi ya kizazi cha sasa na cha huko baadae, na kama inavyoelekeza kwenye Kif 108. Kinavyoashiria kua kuna Sheria inahitajika kutungwa hapo baadae katika usimamizi mzuri wa mapato hayo.

## UKOMO WA SHUGHULI ZA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA

**Mheshimiwa Spika,**

Sehemu hii ina vifungu 7 kuanzia cha 110 hadi 117. Ambayo inaelezea masharti ambayo Kampuni na Mkandarasi wataeleza mpango wa ukomo wa mradi na masharti yaliyowekwa na Sheria hii ni mazuri kwani Kampuni na Mandarasi atalazimishwa kupeleka mpango huo miaka mitano kabla ya shughuli hiyo kufungwa hii, itasaidia Serikali kujua ni maeneo gani ya kuyasimamia kwa karibu ili kuhakikisha mradi ukimalizika basi maeneo hayo yanaendelea kutumika kwa shughuli nyingine za kiuchumi na kijamii.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuhakikisha mpango huo wa ukomo unakua unadhibitiwa baada shughuli kukamilika Kifungu cha 111 kimewekewa masharti ya kuanzishwa kwa mfuko wa Ukomo wa shughuli hizo mafuko ambao utaweza kugharimia shughuli za uondoaji wa miundombinu yote ambayo haitohitajika tena na pia kuyarejesha maeneo katika hali yake ya kawaida ili yaweze kutuika na kwa kuzingatia masharti ya Mazingira. Lakini katika eneo hili tunaiomba Serikali kua makini katika hatua za mwisho kwani Mkandarasi akisha maliza kurejesha gharama zake alizotumia mitambo yote itakua ni mali ya Serikali na mpango huo wa ukomo itabidi uonyeshe ni namna gani inaweza kutumika tena au kuondolewa kabisa.

Mhe Spika hapo jambo kubwa na muhimu ni kuona masuala yote ya uharibifu wa mazingira basi yamedhitiwa ipasavyo kama ilvyoelezwa katika Kif 131 cha SHERIA HII.

## THAMANI YA WADAU

**Mheshimiwa Spika,**

Sehemu hii ina vifungu 5 kuanzia 134 hadi 138, sehemu ambayo inaonyesha ni jinsi gani wanachi wa kawaida watafaidika moja kwa moja na shughuli hizi za Mafuta na Gesi kwa

kusaidia jamii kwenye Elimu, Afya, Maji safi na Salama, kushirikiana na wafanya biashara Wazalendo katika kuinua na kuzitumia bidhaa zao, kutoa kipau mbele kwa bidhaa zinazozalishwa ndani ya Nchi, pamoja na mambo mengine ya kijamii.

Mhe Spika, eneo hili ni gumu kulifahamu lakini kimsingi kwa uzoefu wa Nchi nyingi basi sisi tuko vizuri. Na tayari wapo Makampuni wameonyesha nia ya kukubaliana na masharti hayo na mengine mazuri zaidi kwa Nchi yetu.

## MAKOSA NA ADHABU

**Mheshimiwa Spika,**

Sehemu hii ina vifungu 11 kuanzia 139 hadi 146 Kamati yangu katika sehemu hii haina pingamizi nayo kwani adhabu zilizotajwa zimezingatia ukubwa na uzito wa masuala haya ya Mafuta na Gesi.

## UTATUZI WA MIGOGORO

**Mheshimiwa Spika,**

Sehemu hii ina vif 4 kuanzia 147 hadi 150 inazungumzia utatuzi wa migogoro sehemu hii inaelezea iwapo kutatokezea utata kwa Kampuni baina yao ambazo hazihusiani na Serikali Mmalaka itaweza kuingilia kati na kuleta suluhu kwa mujibu cwa Kanuni zitakazotungwa.

## MASHARTI YA MPITO

**Mheshimiwa Spika,**

Sehemu hii iko katika Kifungu cha 151 kifungu hiki Kamati kwa jinsi kilivyo kamati yangu hakijaridhika na jinsi kilivyo ila tunaomba kurekebishwe na kuondoa neno haitokuwa na wajibu badala ya neno Serikali na liongezwe nano haitofugwa na Mikataba yoyote iliyoingiwa hapo nyuma.

## MASHARTI YA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,**

Sehemu hii ina vifungu 4 kuanzia kifungu cha 152 hadi 155. Aidha, kifungu cha 154 kinaelezea kuanzisha Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Petroli, Sheria hii ndio itakayokua msimamizi mkuu wa wa mipango yote ya maenedeleo ya sasa na ya hapo baadae na hiki ndicho kilio chetu kikubwa wajumbe na tunaiomba Serikali kuhakikisha Sheria hiyo inakuja hapa Barazani hivi karibuni ili kuweza kutimiza lengo la Sheria hii na kama Sera inavyoleza.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati yangu inaishauri Serikali yetu katika hiyo mipango ya baade katika kuimarisha uchumi wa Zanzibar kupitia mfuko wa maendeleo ya Petroli hapa Zanzibar kuangalia kukuza na kulinda utalii wetu , kuanzisha viwanda vya kusindika Samaki, kuimarisha Sekta nzima ya Uvuvi, kuimarisha miundombinu ya Kilimo hasa kuchimba visima na kujenga miundombinu ya umwagiliaji ili tujitosheleze na chakula na kuuza cha ziada, kujenga na kuimarisha miundombinu katika sekta ya ICT , kujenga na kuviimarisha vyuo vya Amali, kuimarisha makaazi ya watoto yatima na wazee wasiojiweza, kuanzisha Shirika la Ndege na kunua Ndege zake yenyewe ,kuimarisha usafiri wa Baharini , kununua vifaa vya kisasa kwa vikosi vyetu vya SMZ , ili kuimarisha ulizni wetu wa Baharini na nchi kavu pia kuimarisha maeneo huru ya kiuchumi na kuanzisha viwanda vidogo vidogo na vya kati ili kuongeza ajira kwa vijana wetu , vile vile kuimarisha sekta ya ujenzi wa makaazi ya wananchi wetu mijini na vijijini pamoja na kuboresha vyuo vyetu na vifaa ili kutoa wataalam wengi wa fani mbali mbali hapa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Kama Sera inavyosema kua wananchi wamejenga matarajio makubwa sana kupitia sekta hii jambo ambalo la kuwaomba wananchi wetu ni kuwa wamoja na kuweka pembeni tofauti za kisiasa kwani bila ya utulivu wa kisiasa haya yote yatakua ni ndoto tu , baada ya hayo naomba sasa kwa niaba ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kuendelea kuwashukuru tena Wajumbe wangu wote wa Kamati pamoja na Wajumbe wa Baraza lako kwa umakini wao wakati wote wa uwasilishaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya wananchi wa Shaurimoyo naunga mkono mswaada huu na naomba kuwasilisha.

**Ahsante**

……………………….

**Hamza Hassan Juma**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar.**